

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA HUDUMA ZA
NISHATI NA MAJI
(EWURA)**

TAARIFA KWA UMMA

(Imetolewa chini ya kifungu Na. 7 (1) na 23 cha sheria ya Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji, Sura ya 414 na kifungu Na. 4 kuhusiana na biashara ya Mafuta, Sura ya 392 ya Sheria za Tanzania)

Taarifa inatolewa kwa wadau wote wa sekta ya Mafuta ya Petroli kwamba katika kutekeleza majukumu yake yaliyoainishwa katika sheria ya EWURA sura ya 414 na ile ya Sheria ya Mafuta ya Petroli sura ya 392, EWURA iko kwenye mchakato wa kuandaa leseni za biashara za jumla na za rejareja katika sekta ya mafuta ya petroli. Rasimu ya leseni hizo itakapopitishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya EWURA itanza kutumika rasmi ifikapo Julai 1, 2007.

Katika jitihada za kuboresha utawala bora na kwa mujibu wa kifungu Na. 23 Sura ya 414 ya Sheria ya EWURA, EWURA inao wajibu wa kuwashirikisha wadau wake katika kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na uandaaji na utoaji wa leseni.

Kwa hiyo basi, mtu yeyote au Taasisi inayotaka kutoa maoni na kuongezea lolote katika leseni hizo anaweza kupata rasimu ya Leseni hizo katika ofisi ya EWURA na kuleta maoni yake kwa kufika au kuandikia ofisi ya EWURA kupitia kwa Mkurugenzi Mkuu kwa anwani iliyotajwa hapa chini kabla ya tarehe saa 11 jioni tarehe 31 May 2007.

Mkurugenzi Mkuu
Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA)
Barabara ya Samora Ghorofa ya 6, Harbour View Towers
(Zamani Jengo la JM Mall)
S.L.P 72175
DAR ES SALAAM
SIMU NAMBA: (+255-22) 2123850; 2123854; 2123856
NUKSHI: (+255-22)